

K: Kusoma.
K: Kuandika.
K: Kuhesabu.

## SHULE YA MSINGI NYAMIHINI

### Historia ya Shule.

Shule ya Msingi Nyamihini ni miongoni mwa shule za msingi zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe Mkoa wa Kigoma. Shule hii ilianzishwa mwaka 2002 ikiwa na Wanafunzi 95 wa daras la Kwanza. Ilianza na Walimu 2 na sasa ina jumla ya walimu kumi na moja (Me 5 na Ke 6).

**UANDIKISHWAJI KWA MIAKA 5 MFULULIZO.**

| MWAKA | WAVULANA | WASICHANA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 2013 | 27 | 25 | 52 |
| 2014 | 25 | 29 | 54 |
| 2015 | 37 | 33 | 70 |
| 2016 | 38 | 34 | 72 |
| 2017 | 70 | 73 | 143 |

# MABORESHO YA MTAALA WA ELIMU KWA SHULE ZA MSINGI.

## *FAIDA ZA MTAALA MPYA.*

01 Mtaala huu ulioboreshwa umejikita zaidi katika utendaji.Hivyo huwapatia wanafunzi fursa ya kutenda zaidi.

02 Kusheheni kwa machapisho darasani kunawafanya wanafunzi kuwa wadadisi na kujifunza kwa urahisi.

03 Kupitia mtaala huu ulioboreshwa imesaidia wanafunzi kupunguziwa mzigo wa masomo kutoka masomo saba (7) hadi kufikia masomo matatu (3) tu.

04 Kuondolewa kwa somo la Kingereza kumehamasisha wanafunzi kumudu stadi za K.K.K kwa urahisi zaidi.

05 Mbinu na njia zinazotumika zimewafanya wanafunzi wajifunze kwa urahisi zaidi. Mbinu shirikishi, Nyimbo za Kuhesabu kwa Vitendo.


Mkoa Wa Kigoma.
Halmashauri ya Wilaya Ya Buhigwe

+255 717 706 441

www.buhigwedc.go.tz


2017 (C) Tehama Buhigwe

# K.K.K

Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

## Kujua K.K.K

Kabla ya mtaala ulioboreshwa wanafunzi wengi walimudu K.K.K kwa uhakika kuanzia darasa III, lakini sasa uwepo wa mtaala huu ulioboreshwa umepelekea wanafunzi wamudu stadi za K.K.K wakiwa darasa la I.

equip Tanzania
Education Quality Improvement Programme



HALMASHAURI YA WILAYA BUHIGWE



# CHANGAMOTO:

## Kutokana na Mtaala ulioboreshwa.

01 Kutopatikana kwa wakati vitabu vya mtaala mpya mathalani vitabu vya darasa la tatu 2017.

02. Upungufu wa vitabu vya Mtaala mpya mathalani vitabu vya Darasa la nne hadi sasa havijafika.

03. Upungufu wa walimu katika shule, Uwiano sahihi ni 1:45 (Mwalimu mmoja kwa wanafunzi arobaini na tano), lakini kwa shule ya misingi Nyamihini ni tofauti, darasa la kwanza ni 1:143 (Mwalimu mmoja Kwa Wanafunzi mia moja arobaini na tatu).

04. Idadi kubwa ya wanafunzi darasani, mathalani katika shule ya Msingi Kilelema, darasa la kwanza lina jumla ya wanafunzi 393.

05. Walimu kutohudhuria mafunzo kwa wakati mmoja. Hii inasababisha kupunguza ufanisi katika kutekeleza mtaala mpya katika shule husika.

06. Uhaba wa miundombinu hasa vyumba vya madarasa kuendana na idadi kubwa ya wanafunzi.

# UFUMBUZI WA CHANGAMOTO:

01 Kugawa darasa katika Awamu kuu mbili (Asubuhi hadi jioni), Awamu ya kwanza kuanzi saa 2:00 - 5:00 na awamu ya pili saa 5:00 hadi 8:30.

02. Walimu kutumia mbinu shirikishi kwa kuwagawa wanafunzi katika vikundi, na mwalimu kupitia kila kikundi.

03. Kufanya utaratibu wa kutoa machapisho kutokana na Muongozo wa mtaala mpya.

04. Walimu wachache waliokwenda kwenye mafunzo kupanga ratiba ya kujengeana uwezo kwa walimu wenzao.

# MAONI NA USHAURI:

Mtaala mpya kabla ya kuanza kutumika ni vyemavifaa vyake vyote vikaandaliwa kwa wakati.



Mtoto **Amos Amoni** wa darasa la Kwanza akipongezwa na wanafunzi wenzake baada ya kusoma kwa ustadi **K.K.K.**



# K.K.K

**Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.**